OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA

SHULE YA SEKONDARI LYASA,
S.L.P 1031,
IRINGA
SIMU- 0784 764092

KUMB NA ED/LYSS/USAJ/VOL-I/30 11.12.2020

KWA …….

……..

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI LYASA WILAYA YA IRINGA MKOA WA IRINGA MWAKA 2021

1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021. Shule ya sekondari Lyasa ipo umbali wa km 72 kusini mwa mji mkuu wa mkoa/halmashauri ya IRINGA. Usafiri wa basi kutoka mjini Iringa unapatikana stendi kuu. Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe 11.01.2021. unatakiwa kuripoti shuleni siku hiyo ya kufungua shule bila kukosa.

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 SARE ZA SHULE

(a) WAVULANA

Suruali mbili rangi ya khaki, Shati mbili nyeupe mikono mirefu, Sweta damu ya mzee mbili, Soksi nyeusi pea mbili na Viatu vyeusi vya kamba visigino vifupi.

Sare ya baada ya masomo

Suruali mbili rangi damu ya mzee na T-shirt za bluu ya kuiva mbili.

Sare ya michezo

Track suit ya bluu ya kuiva mkanda mweupe pembeni.

(b) WASICHANA

Sketi mbili rangi ya khaki, mshono rinda box, Shati nyeupe mikono mirefu mbili, Sweta rangi damu ya mzee mbili, Soksi nyeupe pea mbili na Viatu vya kamba visigino vifupi vyeusi.

Sare baada ya masomo

Sketi mbili rangi damu ya mzee na T-shirt za bluu ya kuiva mbili. Aidha rangi ya hijabu kwa wasichana waislamu ni nyeupe.

Sare ya michezo

Track suit ya bluu ya kuiva mikanda mweupe pembeni.

2.2 Mahitaji ya darasani

Daftari 10 aina ya kaunta, Kalamu za wino 5, penseli 5, Mkebe wa hesabu na Kamusi ya lugha ya kiingreza.

Aidha mzazi au mlezi mnunulie mtoto mahitaji ya kutosha kama sabuni, mafuta ya kupaka, miswaki na dawa ya meno, nguo za ndani,kitana,brash ya viatu na dawa ya viatu(kiwi).

3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha , inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi yenye dhamana ya elimu nchini na TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala mara baada ya kuripoti shuleni.

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.

(c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya join (preparation)
(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
(f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mzingira ya shule.
(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
(i) Kutunza mali za umma.

3.1 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

(a) Wizi
(b) Uasherati na ushoga
(c) Ubakaji
(d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kuberi, nk.
(e) Kupigana au kupiga
(f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
(g) Kudharau Bendera ya Taifa.
(h) Kuwa mjamzito/ kupata mimba.
(i) Kuoa au kuolewa
(j) Kutoa mimba.
(k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
(l) Kukataa adhabu kwa makusudi.
(m) Kuwa na simu ya mkononi.

4.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI

(a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
(b) Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
(c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
(d) Uje na kivuli cha cheti cha kuzaliwa.

Tafadhari soma kwa umakini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI LYASA
Ahsante

.....
Mwl. Kilundo,D.R.
MKUU WA SHULE

OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA
SHULE YA SEKONDARI LYASA

FOMU YA UKIRI WA KWENDA SHULE ALIYOPANGIWA MWANAFUNZI

A. TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI

JINA ..... JINSIA ..... DINI .....

UMRI .....URAIA .....KABILA .....

ANUANI YA NYUMBANI .....

SHULE YA MSINGI ULIYOTOKA .....

B. UKIRI

MIMI .....NAKIRI KUWA NIMESOMA NA KUELEWA MAELEKEZO YOTE YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI LYASA. NA KWAMBA SITALETA MGOMO AU KUSHAWISHI WENZANGU KUGOMA HIVYO NAKUBALI KUJIUNGANA SHULE KIDATO CHA ..... MWAKA .....

SAINI ..... TAREHE .....

C. MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI

MIMI .....AMBAYE NI MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI AITWAYE ..... NIMEKUBALI KUMHUDUMIA MWANANGU/MWANAFUNZI HUYU KWA KUMPA MAHITAJI YOTE ILI KUMWEZESHA KUSOMA VIZURI SHULENI

ANUANI YANGU NI .....

NAMBA YA SIMU NI .....

KAZI YANGU NI .....

SAINI ..... TAREHE .....

MUHIMU: JAZA FOMU HII NA IRUDISHWE SHULENI SIKU YA KURIPOTI SHULENI

PRESIDENT'S OFFICE REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

IRINGA DISTRICT COUNCIL

LYASA SECONDARY SCHOOL,
P. O. BOX 1031,
IRINGA
MOB: 0784 764092

REF: NO.ED/LYSS/USAJ/VOL1/31 11.12.2020

TO MEDICAL OFFICER

…….....……

……..

Dear sir/madam

REF: MEDICAL EXAMINATION TO OUR STUDENT CALLED

.....

Please examine the above named student as to whether she/he is fit to join secondary school studies.

MEDICAL OFICER'S CERTIFICATION

(This area is to be completed by medical officer)

The named student above is fit/not fit for studies due to (state reasons)

.....

.....

Name ..... Signature.....

Station ..... Designation .....

Date .....